BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2019

## 612 URAIA

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2019

## 612 URAIA

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


1.0 UTANGULIZI ........................................ 1

2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI ........................................ 2

2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Utaalamu) ........................................ 2

2.1.1 Swali la 1: Dola ........................................ 2

2.1.2 Swali la 2: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Uraia ........................................ 4

2.1.3 Swali la 3: Dola ........................................ 6

2.1.4 Swali la 4: Uchambuzi wa Machapisho/Maandiko muhimu ya kufundishia na kujifunzia somo la Uraia ........................................ 9

2.1.5 Swali la 5: Utamaduni Wetu ........................................ 11

2.1.6 Swali la 6: Zana za Kufundishia na Kujifunzia somo la Uraia ........................................ 13

2.1.7 Swali la 7: Uhusiano wa Kimataifa ........................................ 16

2.1.8 Swali la 8: Uchambuzi wa Machapisho/Maandiko Muhimu ya kufundishia na kujifunzia Somo la Uraia ........................................ 19

2.1.9 Swali la 9: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia ........................................ 21

2.1.10 Swali la 10: Upimaji na Tathmini ........................................ 23

2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma) ........................................ 25

2.2.1 Swali la 11: Dola ........................................ 25

2.2.2 Swali la 12: Utamaduni wetu ........................................ 29

2.2.3 Swali la 13: Uchumi wa Tanzania ........................................ 34

2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha (Utaalamu) ........................................ 38

2.3.1 Swali la 14: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Uraia ........................................ 38

2.3.2 Swali 1a 15: Zana za kufundishia na Kujifunzia ........................................ 42

2.3.3 Swali la 16: Upimaji na Tathmini ........................................ 46

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA ........................................ 51

4.0 HITIMISHO ........................................ 52

5.0 MAPENDEKEZO ........................................ 53

Kiambatisho ........................................ 54

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linayo furaha kutoa taarifa ya watahini kuhusu ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kuhitimu Ualimu Daraja la Tatu A kwa somo la Uraia. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu kwa wanachuo, wakufunzi, waandaaji sera na wadau wa elimu kwa ujumla.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho ambayo pamoja na mambo mengine, inaonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia. Kimsingi majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa kipi mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa watahiniwa walipokuwa katika mafunzo ya Ualimu katika daraja hili.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za watahiniwa kufanya vibaya au vizuri katika mtihani wao. Mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, wakuu wa vyuo, wakufunzi na wanavyuo kupata mbinu muafaka katika kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Mwisho, Baraza linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, Watahini wa somo na wadau wote waliohusika katika uchambuzi wa takwimu na kutayarisha taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la **612 Uraia** kwa watahiniwa wa Ualimu ngazi ya Astashahada uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Uraia wa mwaka 2009 na fomati ya Mitihani ya mwaka 2017.

Mtihani ulikuwa na maswali kumi na sita (16) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu jumla ya maswali kumi na nne (14) kutoka katika sehemu **A**, **B** na **C**. Sehemu A, ilikuwa na maswali kumi (10) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote, ambapo kila swali lilikuwa na alama nne (04). Sehemu B na C zilikuwa na maswali matatu (03) kila moja, ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili kutoka katika kila sehemu. Kila swali katika sehemu B na C lilikuwa na alama 15.

Ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa Uraia kwa mwaka 2019 ulikuwa wa kiwango kizuri ambapo asilimia **100** ya watahiniwa waliofanya mthani walipata wastani wa alama 40 au zaidi. Kati yao asilimia 0.6 walipata daraja A, asilimia 21.6 daraja B, asilimia 75.4 daraja C na asilimia 2.3 daraja D. Ufaulu wa watahiniwa umegawanywa katika viwango vitatu ambavyo ni 'vizuri', 'wastani', na 'hafifu'. Ufaulu wa kiwango kizuri unaanzia alama 70 hadi 100; kiwango cha wastani alama 40 hadi 69; na kiwango hafifu alama 0 hadi 39. Aidha, chati za viwango vya ufaulu zimeambatishwa ili kufafanua ufaulu wa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu wa kiwango kizuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa kiwango cha wastani na rangi nyekundu inawakilisha ufaulu wa kiwango hafifu.

Taarifa hii inachambua maswali yenye ufaulu mzuri, wa wastani na hafifu ili kukuza kiwango cha ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia. Uchambuzi huu unalenga kuonesha jinsi watahiniwa walivyojibu maswali katika mtihani wa Uraia. Sampuli za majibu yao zimeambatishwa ili kuonesha kilichofanywa na watahiniwa. Aidha, taarifa inaonesha sababu zilizowafanya watahiniwa wachache kutopata alama za juu katika majibu ya maswali katika baadhi ya mada. Hivyo, uchambuzi huu utasaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia kwa mada hizo ili kuboresha ufaulu kwa watahiniwa katika mitihani yao.


## 2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI

## 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Utaalamu)

Katika sehemu hii kila swali lilikuwa na jumla ya alama 4. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu, ambapo mtahiniwa alikuwa na kiwango hafifu, wastani na kizuri cha ufaulu endapo alipata kuanzi alama 0 hadi 1.5, 2 hadi 2.5 na 3 hadi 4, mtawalia.


### 2.1.1 Swali la 1: Dola

Katika swali hili, watahiniwa walitakiwa kuonesha kwa hoja nne namna gani raia wanaweza kushiriki katika Serikali za Mitaa. Kati ya watahiniwa 4,787 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 43 (0.9%) walipata ufaulu hafifu wa kuanzia alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 49 (1.0%) walikuwa na ufaulu wa wastani wa kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 4,695 (98.1%) walipata ufaulu mzuri wa kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa asilimia 99.1 ya watahiniwa waliweza kupata alama 2 hadi 4 ambao ni ufaulu wa wastani hadi mzuri. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 1:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 1*

Watahiniwa waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Dola*, hususan kipengele cha *Serikali za Mitaa*. Watahiniwa hao walielewa matakwa ya swali hivyo kuweza kutoa hoja sahihi zisizopungua tatu. Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa ni kama vile: *Kushiriki katika maendeleo ya elimu katika kata husika, kama vile kushiriki katika ujenzi wa shule, kupiga vita uhalifu katika kata, kama vile kushirikiana na polisi katika kudumisha ulinzi na usalama wa Kata, kushiriki katika chaguzi mbalimbali, kushiriki katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali, kama vile shule, zahanati,* n.k. Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.


01. Raia wanawezo kushiriki katika serikali za mitaa kwa njia mbalimbali kama ifuatavyo:
(i) Kulipa kodi na michango mbalimbali inayolenga kuendeleza maendeleo katika mtaa inapobidi
(ii) Raia wanawezo kushiriki kuchagua viongozi mbalimbali katika ngazi ya serikali za mtaa Mfano, Diwani wa kata na Mwenyekiti wa kijiji
(iii) Kushiriki katika miradi mbalimbali ya kimaendeleo katika mitaa kama vile kufanya usafi wa mazingira na kutunza Maliasili
(iv) Kushiriki kufichua wahalifu waliopo ndani ya mitaa Mfano wezi, wabakaji na Mafisadi.


**Kielelezo Na. 1.1:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

Katika Kielelezo Na. 1.1 mtahiniwa alionesha kwa usahihi namna raia wanavyoweza kushiriki katika Serikali za Mitaa, hivyo alipata alama za juu.

Watahiniwa waliopata kuanzia alama 2 hadi 2.5 walionesha kuwa na maarifa ya wastani kuhusu mada ndogo ya *Serikali za Mitaa*. Watahiniwa hawa walitoa hoja pungufu ya hoja nne zilizohitajika katika swali. Wengine

kati yao, walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Miongoni mwao, waliokuwepo waliorudia hoja zaidi ya mara moja hivyo, kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja, mbali na hoja sahihi alizotoa, pia alichanganya na hoja kama vile: *kutoa michango ya shule* na *kuweka walinzi wa usalama* ambazo si sahihi, hivyo kumsababishia kupata alama za wastani.


Aidha, watahiniwa wachache (0.9%) waliopata alama hafifu katika swali hili, baadhi yao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana nzima ya Serikali za Mitaa. Hii iliwasababishia kutoa majibu mchanganyiko, sahihi na yasiyosahihi, hivyo kupata alama hafifu. Wengine walidhihirisha kutoelewa matakwa ya swali, hivyo kutoa majibu yasiyokuwa na uhusiano na swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alionesha sifa anazotakiwa kuwa nazo mtu anayetaka kugombea nafasi ya uongozi wa mtaa badala ya kuonesha ushiriki wa raia katika Serikali za mitaa kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 1.2.


Namna ambavyo raia wanaweza kushiriki kati
ka Serikali za mitaa ni :-
i> kutimiza miaka 18 na kuendelea
ii> Awe na akili timamu
iii> Awe na kitambulisho cha Utaifa
iv) Awe anaweza kusoma na kuandika

**Kielelezo Na. 1.2:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.


### 2.1.2 Swali la 2: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Uraia

Swali hili liliwataka watahiniwa kubainisha vipengele vinne vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vyenye uhusiano na mada mbalimbali za somo la Uraia. Swali hili lilifanywa na watahiniwa wote 4,787 (100%), kati yao watahiniwa 944 (19.7%) walikuwa na ufaulu hafifu wa kuanzia alama 0 hadi 1.5 na watahinwa 633 (13.2%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata kuanzia alama 2 hadi 2.5. Aidha, watahiniwa 3,210 (67.1%) walikuwa na ufaulu mzuri wa kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa asilimia 80.3 ya watahiniwa waliweza kupata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 2.




**Chati Na. 2:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 2*


Watahiniwa waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 waliweza kubainisha vipengele visivyopungua vitatu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vyenye uhusiano na mada mbalimbali za somo la Uraia kama vile: *Haki za binadamu*, *Majukumu ya Rais*, *Demokrasia*, *majukumu ya Bunge*, *Ulinzi na Usalama*, *Baraza la Mawaziri na Majukumu yake*, n.k. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ndogo ya *Uhusishi wa mada za Uraia na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*, hivyo walielewa vyema matakwa ya swali. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mmoja wa watahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.




**Kielelezo Na. 2.1:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa majibu sahihi.

Katika Kielelezo 2.1 mtahiniwa alibainisha vipengele vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vyenye uhusiano na mada mbalimbali za somo la Uraia kwa ufasaha, hivyo alipata ufaulu mzuri.

Aidha, wengi kati ya watahiniwa (19.7%) waliopata kuanzia alama 0 hadi 1.5, walishindwa kuelewa matakwa ya swali kwa kueleza aidha *muundo, ibara* au *sura za katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania* badala ya vipengele vya katiba vinavyohusiana na mada mbalimbali katika somo la Uraia, hivyo kuwasababishia kupata alama 0. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile: *Ibara ya 210, ibara ya 10, ibara ya 120, ibara ya 21;* na mwingine aliandika: *Kipengele namba tisa, kipengele namba mbili, kipengele namba sita na kipengele namba moja*. Watahiniwa wengine katika kundi hili walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Katiba*, hivyo kuwafanya watoe hoja dhaifu zilizopelekea kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili.



2. Vipengele vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano
i/ Kichwa cha katika
ii/ Utangulizi au yaliyomo
iii/ Sura
iv/ Ibara

**Kielelezo Na. 2.2:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeenda kinyume na matakwa ya swali.

Katika Kielelezo Na. 2.2 mtahiniwa alijaribu kutaja muundo wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania badala ya vipengele vya Katiba vinavyohusiana na mada mbalimbali katika somo la Uraia kama vile; *Majukumu ya Rais*, *Demokrasia, majukumu ya Bunge*, *Ulinzi na Usalama*, *Baraza la Mawaziri na Majukumu yake*, n.k.


### 2.1.3 Swali la 3: Dola

Katika swali hili, watahiniwa walitakiwa kuonesha umuhimu wa uhuru wa Mahakama kwa kutoa hoja nne. Kati ya watahiniwa 4,787 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 3,093 (64.6%) walipata ufaulu hafifu wa kuanzia alama 0 hadi 1, watahiniwa 671 (14%) walipata ufaulu wa wastani wa alama 2 na watahiniwa 1,023 (21.4%) walipata ufaulu mzuri wa kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kuwa ni asilimia 35.4 tu ya watahiniwa ndio waliweza kupata alama 2 hadi 4, kama inavyoonekana katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 3*


Wengi kati ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 0 hadi 1, walichanganya dhana kwa kutaja majukumu au kazi za mahakama au umuhimu wa kuwa na mahakama badala ya kueleza umuhimu wa uhuru wa mahakama. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile: *Kutafsiri sheria, kulinda katiba ya nchi, kulinda sharia za nchi na kuamua kesi mbalimbali*, majibu ambayo hayakuwa sahihi, hivyo kumsababishia kupata alama 0. Wengine katika kundi hili walidhihirisha kuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana ya *uhuru wa Mahakama*, hivyo kuwafanya watoe majibu yasiyo na uhusiano na swali au kuchanganya majibu sahihi na yasiyosahihi. Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.


3 i/ kufitetea
ii/ kutolewa ushahidi
iii/ kuopiwa iv) kutolewa dhamana

**Kielelezo Na. 3.1:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu hafifu.

Katika Kielelezo Na. 3.1 mtahiniwa aliandika mambo ambayo hayana uhusiano na umuhimu wa uhuru wa mahakama. Mtahiniwa alitaja istilahi mbalimbali zinazotumika Mahakamani, hivyo alipata alama 0.

Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa watahiniwa waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 katika swali hili walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Dola* hasa mada ndogo ya *Mahakama*. Kwa hiyo waliweza kutoa hoja sahihi zisizopungua tatu, kama vile: *kutocheleweshа haki bila sababu ya msingi*, *kuweza kutenda haki kwa watu wote*, *kuweza kutoa fidia sahihi kwa watu walioathirika kutokana na makosa mbalimbali*, n.k. Watahiniwa hawa, pia walielewa vyema matakwa ya swali, hivyo waliweza kutoa majibu sahihi. Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.



3 (i) Husaidia mahakama kutekeleza kwa usahihi misingi ya katiba ya jamhuri ya muungano wa Tanzania.
(ii) Husaidia kutoa huduma ya haki sawa ya kesheria kwa raia wote bila ubaguzi.
(iii) Husaidia kuondoa na kutatua migogoro mbalimbali mfano katika jamii, migogoro ya mauaji katika vyombo vya dora.
(iv) Husaidia mahakama kufanya kazi yake kwa usahihi pasipo kuingiliwa na mihimili mingine ya dola iliyokuwa yake.

**Kielelezo Na. 3.2:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali.

Kwa upande mwingine, watahiniwa (14%) waliopata alama za wastani katika swali hili, walidhihirisha kuwa na mapungufu mbalimbali kama vile: uchanganyaji wa hoja sahihi na zisizo sahihi, utoaji wa hoja pungufu na kurudia hoja zenye maana moja. Watahiniwa hawa walionesha kuwa na maarifa ya wastani katika mada husika, hivyo kushindwa kutoa hoja sahihi zaidi ya mbili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja baada ya kutoa hoja mbili sahihi, alitoa pia hoja kama vile: *Dora* na *Kuheshimu Katiba* ambazo si sahihi, hivyo kumsababishia kupata alama za wastani.

### 2.1.4 Swali la 4: Uchambuzi wa Machapisho/Maandiko muhimu ya kufundishia na kujifunzia somo la Uraia


Swali hili liliwataka watahiniwa kutaja mambo manne ya kuzingatia katika kutumia kitabu cha kiada. Watahiniwa 4,787 (100%) walifanya swali hili. Kati yao watahiniwa 4,681 (97.8%) walikuwa na ufaulu hafifu wa kuanzia alama 0 hadi 1, watahiniwa 677 (1.4%) walikuwa na ufaulu wa wastani wa kuanzia alama 2 na watahiniwa 39 tu (0.8%) walipata ufaulu mzuri wa kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kuwa ni asilimia 2.2 tu ya watahiniwa ndio walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 4*

Watahiniwa wengi (97.8%) waliopata kuanzia alama 0 hadi 1 katika swali hili, hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo kuwafanya wapate alama 0. Kwa mfano, wapo waliotaja sifa za kitabu cha kiada badala ya mambo manne ya kuzingatia katika kutumia kitabu cha kiada kwa kutoa hoja kama vile: *kiwe na lugha inayoeleweka*, *kisioneshe ubaguzi wa kijinsia*, n.k. Watahiniwa wengine waliandika mambo ya kuzingatia katika kuchagua mbinu ya kufundishia na kujifunzia kwa kutoa hoja kama vile: *kuzingatia mazingira*, *kuzingatia umri wa wanafunzi*, *uelewa wa wanafunzi katika mada* na *lengo mahususi*. Aidha, watahiniwa wengine walidhihirisha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maandiko muhimu ya kufundishia

na kujifunzia somo la Uraia, ambayo iliwasababishia kutoa hoja dhaifu zilizopelekea kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutaja mambo ya kuzingatia katika kutumia kitabu cha kiada.



4. - Mwandishi wa kitabu.
- Mahali kilipochapishwa.
- Mwaka.
- Somo na darasa.

**Kielelezo Na. 4.1:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.

Katika Kielelezo Na. 4.1 mtahiniwa alijaribu kuonesha mtiririko wa kufuata katika kunukuu rejea badala ya mambo ya kuzingatia katika kutumia kitabu cha kiada, hivyo alipata ufaulu hafifu.

Watahiniwa 677 (1.4%) waliopata alama 2 walielewa matakwa ya swali isipokuwa walikuwa na maarifa ya wastani kuhusu mada ya *Maandiko muhimu ya kufundishia na kujifunzia somo la Uraia*. Baadhi yao walishindwa kutoa hoja tatu hadi nne kwa usahihi na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja baada ya kutoa hoja mbili sahihi, alichanganya na hoja kama vile: *idadi ya wanafunzi* na *mada ndogo na kubwa*, ambazo si sahihi.


Watahiniwa wachache (0.8%) waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Uchambuzi wa Maandiko muhimu ya kufundishia na kujifunzia somo la Uraia*. Kwa hiyo waliweza kutoa hoja sahihi, kama vile: *Kila unapofundisha, hakikisha wanafunzi wako wana vitabu vya kiada ili kuweza kufuatilia somo, kila darasa lifundishwe na kitabu cha darasa lao, kwa mfano darasa la Tatu wafundishwe na kitabu cha Darasa la Tatu, kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na kitabu chake cha kiada, hakikisha wanafunzi wana maarifa ya awali na wanachotakiwa kusoma katika kitabu cha kiada, n.k.* Sababu nyingine ya wanafunzi hawa kutoa majibu sahihi ni kuwa, hoja ya kitabu cha kiada hufundishwa kwenye masomo mengine wanayojifunza, hivyo ilikuwa rahisi kwao kuhawilisha maarifa. Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.


4 (i) mwanafunzi lazima awe nacho darasani
(ii) Kiwe na mada zote zilizomo
kwenye muhtasari wa somo la uraia.
(iii) Kiendane na darasa husika.
(iv) Kiwe kinatumika na mwalimu na mwanafunzi
darasani.

**Kielelezo Na. 4.2:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali.


### 2.1.5 Swali la 5: Utamaduni Wetu

Swali hili liliwataka watahiniwa kuorodhesha athari nne za kutokuwa macho na utamaduni wa kigeni nchini Tanzania. Miongoni mwa watahiniwa 4,787 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 42 (0.9%) walipata ufaulu hafifu wa kuanzia alama 0 hadi 1. Watahiniwa 46 (0.9%) walipata ufaulu wa wastani wa kuanzia alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 4,699 (98.2%) walijibu vizuri swali na kupata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni mzuri kwa kuwa asilimia 99.1 waliweza kupata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 5.




**Chati Na. 5:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 5*

Watahiniwa wengi waliopata ufaulu mzuri (98.2%) waliweza kuoredhesha athari zisizopungua tatu za kutokuwa macho na utamaduni wa kigeni nchini Tanzania. Watahiniwa hao walionesha kuelewa matakwa ya swali na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Utamaduni Wetu*. Kwa hiyo waliweza kutoa majibu sahihi kama vile: *Vijana kushindwa kuthamini kazi katika jamii, kufifia kwa mila za Kitanzania, kupotea kwa upendo, uzalendo, kuheshimiana na kushirikiana katika jamii, kuporomoka kwa maadili na tabia njema kwa vijana, kama vile kuwa na mahusiano ya kimapenzi katika umri mdogo, kuvaa nguo fupi sana*, n.k. Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kupata ufaulu mzuri katika swali hili.


5 i) Kusababisha mmomonyoko wa maadili
ii) Mila na desturi za kitanzania kupotea
iii) Kupotea kwa nguvu kazi
iv) Kupotea kwa lugha ya kiswahili


**Kielelezo Na. 5.1:** Sampuli ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

Katika Kielelezo Na. 5.1 mtahiniwa aliorodhesha kwa usahihi athari za kutokuwa macho na utamaduni wa kigeni nchini Tanzania, hivyo alipata alama za juu.

Baadhi ya watahiniwa wachache (0.9%) waliopata alama za wastani waliandika hoja pungufu ya tatu. Wengine walirudia hoja au kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya hoja kama vile; *kushuka kwa maendeleo* na *kuongezeka kwa ujangili* ambazo hazikuwa majibu sahihi.

Kwa upande mwingine, wengi kati ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 0 hadi 1, hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo walitoa majibu ambayo hayakuwa sahihi. Wapo waliochanganya maarifa, kwa mfano mtahiniwa mmoja alitaja athari za kikoloni kwa hoja kama vile: *kuingizwa kwa elimu ya kikoloni*, *kuuliwa kwa viwanda vya jadi*, n.k, badala ya athari za utamaduni wa kigeni. Wengine walidhihirisha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu athari za utamaduni wa kigeni nchini Tanzania, hivyo kuwasababishia kutoa majibu dhaifu yaliyopelekea kutofanya vizuri katika

swali hili. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya jibu lililojibiwa vibaya na mtahiniwa.



5. > Kuanzishwa kwa vyombo vya habari vya kigeni
> Kuingizwa kwa elimu ya kikoloni
> Kufa kwa viwanda vidogo vidogo vya jadi
> Kuanzishwa kwa dini ya Kiislamu na Kikristo.

**Kielelezo Na. 5.2:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeenda kinyume na matakwa ya swali.

Katika Kielelezo Na. 5.2 mtahiniwa alitaja athari za muingiliano kati ya Afrika na wageni kuanzia karne ya 7 badala ya kuorodhesha athari za kutokuwa macho na utamaduni wa kigeni nchini Tanzania.

### 2.1.6 Swali la 6: Zana za Kufundishia na Kujifunzia somo la Uraia

Swali hili lilikuwa na vipengele viwili. Kipengele (a) kiliwataka watahiniwa kutoa maana ya zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia, na kipengele (b) kiliwataka watahiniwa kutaja aina tatu za zana za kufundishia na kujifunzia kwa kutoa mifano. Miongoni mwa watahiniwa 4,787 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 594 (12.4%) walipata ufaulu hafifu wa kuanzia alama 0 hadi 1, watahiniwa 175 (3.7%) walipata ufaulu wa wastani wa kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 4,018 (83.9%) walipata ufaulu mzuri wa kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 87.6 waliweza kupata kuanzia alama 2 hadi 4 ambao ni ufaulu wa wastani hadi mzuri. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya ufaulu katika swali hili.




**Chati Na. 6:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 6*

Wengi kati ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 waliweza kukidhi matakwa ya swali kwa kuonesha maana na makundi ya zana za kufundishia na kujifunzia. Ufaulu huo ulisababishwa na uelewa mzuri wa watahiniwa katika mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia* kwani mada hii hufundishwa katika masomo mengi wanayojifunza. Watahiniwa hao waliweza kutoa hoja sahihi kwa kipengele (a) kama vile: *Zana ni kifaa/vifaa ambavyo mwalimu huvitumia ili kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji*; na waliweza kutaja makundi ya zana kama vile*: Zana maono mfano; mabango, ramani na ubao na chaki, Zana masikizi mfano; redio na Zana masikizi-maono mfano; televisheni, video na sinema*. Tofauti ya alama katika swali hili ilisababishwa na usahihi wa hoja na mifano iliyotolewa na watahiniwa. Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

6 (a) Ni vifaa vinavyotumika katika kufundishia ili kurahisisha tendo zima la Ufundishaji na Ujifunzaji na kulifanya somo liwe fanisi. Mfano wa zana hizo ni Picha na michoro mbali mbali.


b) i) Zana maono
Hii ni aina ya zana inayotumia mlango wa fahamu macho ili kupata taarifa. Mfano wa zana hizo ni Picha, michoro na vitu halisi mfano Machungwa

ii) Zana masikizi
Zana hii hutumia mlango wa fahamu sikio ili kupata taarifa.
Mfano: Redio, Ngoma, Filimbi na baragumu

iii) Zana masikizi maono
Hutumia milango miwili ya fahamu ili kupata taarifa.
Mfano: Runinga, simu, kompyuta na Projecta

**Kielelezo Na. 6.1:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali.

Wengi kati ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 0 hadi 1, hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo walitoa majibu yasiyoendana na swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja mbinu mbalimbali za kufundishia, kama vile: *Maswali na majibu, majadiliano kwenye vikundi* na *changanya kete* na mwingine alitaja mbinu za kupata zana kwa kutoa hoja kama vile: *Kununua, kuazima, kuokota, michoro,* majibu ambayo yalisababisha apate alama 0. Wengine katika kundi hili walidhihirisha kutokuwa na maarifa juu ya mada ya *Zana*, hivyo kutoa hoja dhaifu hasa kwenye kipengele (b). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika makundi ya zana kama vile: *zana za asili, zana za kisasa* na mwengine alitoa hoja kama vile: *zana za kutengeneza, zana za kuchora* na *zana za kufinyanga*, ambapo yote hayakuwa majibu sahihi. Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.


6. (a) Maana ya Zana za kufundishia na kujifunzia somo la uraia ni njia ambazo hutumiwa na mwalimu kwa wanafunzi ili kuweza kufikia malengo mahususi aliyo kusudia katika ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi darasani.

b/.
i/ Kitabu cha kiada
ii/ Kitabu cha ziada
iii/ Kitabu cha rejea

**Kielelezo Na. 6.2:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyekwenda kinyume na matakwa ya swali.


Katika Kielelezo Na. 6.2 mtahiniwa alitoa maana ya mbinu za kufundishia katika kipengele (a) na kutoa aina za vitabu vinavyotumiwa na mwalimu na mwanafunzi katika kipengele (b) kinyume na matakwa ya swali, hivyo alipata alama 0.

Aidha, watahiniwa waliopata kuanzia alama 2 hadi 2.5 walionesha udhaifu mbalimbali katika majibu yao. Mfano, baadhi yao walishindwa kutoa maana sahihi ya zana za kufundishia na kujifunzia na kutoa aina pungufu za zana, hivyo kuwafanya wapate alama pungufu. Wengine walichanganya aina za zana sahihi na zisizo sahihi na wengine kati yao walitaja zana bila mifano.

### 2.1.7 Swali la 7: Uhusiano wa Kimataifa

Swali hili liliwataka watahiniwa kubainisha viashiria vya utandawazi kwa kutumia hoja nne. Kati ya watahiniwa wote 4,787 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 303 (6.3%) walipata ufaulu hafifu wa kuanzia alama 0 hadi 1.5 na watahiniwa 329 (6.9%) walipata ufaulu wa wastani wa kuanzia alama 2 hadi 2.5. Aidha, watahiniwa wengi (86.8%) walipata ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha

ufaulu kwa kuwa asilimia 93.7 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 7.




**Chati Na. 7:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 7*

Watahiniwa waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 waliweza kubainisha viashiria visivyopungua vitatu vya utandawazi kwa usahihi. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Utandawazi* na walielewa vyema matakwa ya swali. Uelewa mzuri wa watahiniwa katika mada hii ulisababishwa na ukweli kwamba utandawazi ni suala mtambuka na maarifa yake huweza kupatikana katika masomo mengi, makala mbalimbali na hata vyombo vya habari. Majibu sahihi katika swali hili yalikuwa kama ifuatavyo: *Uchumi wa soko huria, ushindani wa kidemokrasia katika siasa, mwingiliano wa utamaduni, kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano, kuimarika kwa sekta ya usafirishaji*, n.k. Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali.

| | |
|---|---|
| 7. | i) Kukua kwa sayansi na teknolojia. |
| | ii) Muingiliano wa Utamaduni. |
| | iii) Ushirikiano wa kimataifa katika nyanja mbalimbali. |
| | iv) Kukua kwa sekta ya mawasiliano. |

**Kielelezo Na. 7.1:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kukidhi matakwa ya swali.

Aidha, watahiniwa 329 (6.9%) walidhihirisha kuwa na maarifa ya wastani kuhusu mada husika, kwa hiyo baadhi yao walichanganya viashiria vya utandawazi na athari za utandawazi. Wengine walitaja viashiria pungufu ya vinne na wengine walirudia kiashiria kimoja kwa lugha nyingine, hivyo kuwasababishia kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, wengi kati ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 0 hadi 1.5, hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa hiyo walichanganya maarifa, kwa mfano mtahiniwa mmoja alitaja athari hasi za utandawazi kwa hoja kama vile; *Kuenea kwa magonjwa, wizi wa mitandao, uvaaji wa nguo fupi,* n.k., hivyo kupata alama 0. Wengine katika kundi hili walionesha kukosa maarifa juu ya mada ya *Utandawazi* hali iliyowasababishia kutoa majibu dhaifu, kwa mfano mtahiniwa mmoja alitoa majibu kama *ongezeko la watu, kuongezeka kwa maasi,* n.k. Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha majibu ya mmoja wa watahiniwa aliyepata ufaulu hafifu.


| | |
|---|---|
| 7. | Viashiria vya utamaduni ni |
| | (i) Mila na desturi |
| | (ii) Ngoma |
| | (iii) Mavazi |
| | (iv) Nyimbo au wimbo wa taifa. |

**Kielelezo Na. 7.2:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.

Katika Kielelezo Na. 7.2 mtahiniwa alitaja nyanja za utamaduni badala ya viashiria vya utandawazi. Hata hivyo, alichanganya na wimbo wa Taifa ambao ni miongoni mwa alama za Taifa, hivyo alipata ufaulu hafifu.

### 2.1.8 Swali la 8: Uchambuzi wa Machapisho/Maandiko Muhimu ya kufundishia na kujifunzia Somo la Uraia

Swali hil liliwataka watahiniwa kutaja sifa nne za malengo mahsusi katika Muhtasari wa somo la Uraia. Kati ya watahiniwa 4,787 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 446 (9.3%) walikuwa na ufaulu hafifu wa kuanzia alama 0 hadi 1. Watahiniwa 334 (7%) walipata ufaulu wa wastani wa alama 02. Watahiniwa 4,007 (83.7%) walipata ufaulu mzuri wa kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni mzuri kwa kuwa asilimia 90.7 waliweza kupata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 8.




**Chati Na. 8:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 8*

Watahiniwa waliopata alama 3 hadi 4 katika swali hili, waliweza kutaja sifa zisizopungua tatu za malengo mahsusi. Watahaniwa hao waliweza kubaini matakwa ya swali na walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika kipengele cha *uchambuzi wa Muhtasari wa somo la Uraia*, hivyo kutoa majibu sahihi, kama vile*: Kuwa na umahsusi katika kile kinachofundishwa, kupimika; yasiwe na kitenzi zaidi ya kimoja, kufikika; viwe ni vitendo vinavyotekelezeka, yawe yakinifu; vitendo vyake vionekane*, n.k. Kielelezo

Na. 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.

| | |
|---|---|
| 8. | Sifa za lengo mahsusi |
| | i) Liwe linapimika. |
| | ii) Liwe na muda maalumu wa kuisha. |
| | iii) Liwe linatekelezeka. |
| | iv) Liwe mahsusi. |

**Kielelezo Na. 8.1:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri.

Katika Kielelezo Na. 8.1 mtahiniwa alitaja sifa za malengo mahsusi katika Muhtasari wa somo la Uraia kwa usahihi, hivyo alipata alama za juu.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa asilimia 9.3 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu hafifu. Wengi kati yao walichanganya maarifa kwa kutaja umuhimu wa malengo mahsusi, vipengele vya Muhtasari au umuhimu wa Muhtasari wa somo la Uraia, hali iliyowasababishia kupata alama 0. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja hoja kama vile: *huonesha zana za kufundishia na kujifunzia*, *huonesha mada kubwa na ndogo*, *huonesha vitendo vya ujifunzaji*, n.k. Mtahiniwa mwingine aliandika; *humsaidia mwalimu kuandaa nukuu za somo, humfikirisha na humsaidia mwalimu kufikia malengo ya somo*. Aidha, watahiniwa wengine walionesha kuwa na maarifa hafifu juu ya mada husika, hivyo kuchanganya jibu sahihi na yasiyo sahihi. Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi katika swali hili.

| | |
|---|---|
| 8 | i) Humbadilisha mlengwa katika kuwa raia mwema |
| | ii) Humtayarisha mlengwa kwa kitu/kazi fulani |
| | iii) Humsaidia kujua namna ya kuishi katika jamii |
| | iv) Humsaidia mlengwa kujua sera mbalimbali za |
| | nchi |


**Kielelezo Na. 8.2:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.

Katika Kielelezo Na. 8.2 mtahiniwa alijaribu kutaja umuhimu wa kujifunza stadi za Uraia badala ya sifa za malengo mahsusi katika Muhtasari wa somo la Uraia.

Aidha, baadhi ya watahiniwa waliopata alama 2 walichanganya sifa za malengo mahsusi na umuhimu wa Muhtasari kwa mwalimu wa Uraia na wengine walitoa hoja pungufu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja, mbali na hoja mbili sahihi alizotoa, pia alitoa hoja kama vile; *lionyeshe mazingira* na *lionyeshe badiliko la hali* ambazo si sahihi.


### 2.1.9 Swali la 9: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia

Swali hili liliwataka watahiniwa kwa kutumia hoja nne, kuonesha umuhimu wa nukuu za somo kwa mwalimu wa somo la Uraia. Watahiniwa wote 4,787 (100%) walifanya swali hili. Watahiniwa 11 (0.2%) walipata ufaulu hafifu wa kuanzia alama 0 hadi 1. Watahiniwa 18 (0.4%) walipata ufaulu wa wastani wa kuanzia alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 4,758 (99.4%) walipata ufaulu mzuri wa kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 99.6 waliweza kupata ufaulu wa wastani hadi mzuri kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 9.




**Chati Na. 9:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 9*

Watahiniwa waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 katika swali hili walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika kipengele *cha nukuu za somo* na walielewa vema matakwa ya swali. Watahiniwa hawa waliweza kuonesha katika hoja zisizopungua tatu umuhimu wa nukuu za somo kwa mwalimu wa somo la Uraia. Baadhi ya hoja sahihi zilikuwa kama ifuatavyo: *Kumwezesha mwalimu kuwa na uhakika na kile anachofundisha, kumsaidia mwalimu kufanya ufafanuzi wa mada darasani, kumkumbusha mwalimu iwapo amesahau kuwasilisha jambo au anataka kurudia, kumsaidia mwalimu kuandaa andalio la somo, kumsaidia mwalimu kufundisha kwa mtiririko mzuri* n.k. Kielelezo Na. 9 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.


9. i) Humsaidia mwalimu kujiamini anapokuwa darasani.
ii) Humsaidia mwalimu kufundisha kwa mtiririko kama aliyopanga.
iii) Humsaidia mwalimu kutotoka nje ya mada.
iv) Humsaidia mwalimu kutumia kama rejea.

**Kielelezo Na. 9:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyefanya vizuri katika swali hili.

Katika Kielelezo Na. 9 mtahiniwa alionesha kwa usahihi umuhimu wa nukuu za somo kwa mwalimu wa somo la Uraia, hivyo alipata ufaulu mzuri.


Kwa upande mwingine, wengi kati ya watahiniwa 18 (0.4%) waliopata ufaulu hafifu katika swali hili, walishindwa kuelewa matakwa ya swali, hivyo kuwafanya watoe majibu tofauti na walichoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja sifa za nukuu bora za kufundishia somo la Uraia kwa kutoa hoja kama vile: *Zenye mtiririko mzuri wa mada*, *zenye ufafanuzi wa maudhui* na *huonesha mazoezi*. Mtahiniwa mwingine alitaja mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa nukuu za somo kwa kutoa hoja kama vile: *Mwalimu kuelewa malengo mahsusi*, *mwalimu kuelewa vyanzo vya maudhui na rejea zitakazotumika* na *kufahamu matumizi ya nukuu zilizoandaliwa*. Aidha, watahiniwa wengine katika kundi hili, walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya *nukuu za somo*, hivyo

kutoa majibu mchanganyiko ambayo mengine hayakuwa na uhusiano na swali, na watahiniwa wengine hawakujibu.

Aidha, watahiniwa waliopata kuanzia alama 2 hadi 2.5 walikuwa na dosari mbalimbali katika majibu yao. Wengi walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na wengine walitoa hoja pungufu au hoja dhaifu, hivyo kushindwa kupata alama za juu.

### 2.1.10 Swali la 10: Upimaji na Tathmini


Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kutaja manufaa ya maswali ya kuchagua katika somo la Uraia kwa kutumia hoja nne. Kati ya watahiniwa 4,787 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 2,558 (53.4%) walipata ufaulu hafifu wa kuanzia alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 971 (20.3%) walikuwa na ufaulu wa wastani wa kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 1,258 (26.3%) walipata ufaulu mzuri wa kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kwa kuwa ni asilimia 46.6 tu ya watahiniwa ndio waliweza kupata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 10.




**Chati Na. 10:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 10*

Watahiniwa waliopata kuanzia alama 0 hadi 1.5 hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo walitoa majibu yasiyo sahihi. Wengi katika kundi hili walitaja faida za kuwa na chaguzi za maswali na kutoa hoja kama vile; *humsaidia*


*mwanafunzi kufanya maswali ambayo yanaeleweka kwa urahisi, humsaidia mwanafunzi kuwa na maamuzi sahihi ya maswali, humsaidia kuchambua maswali vizuri, husaidia kupima utambuzi wa maswali wa mwanafunzi* n.k., hivyo walipata alama 0. Wengine walidhirisha kuwa na maarifa hafifu katika dhana nzima ya *zana za Upimaji katika somo la Uraia*, hivyo baadhi yao walitoa majibu ya kubuni ambayo hayakuwa sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja, alitoa hoja kama vile; *kumsaidia mwanafunzi kujibu kwa haraka, kuokoa muda, kujibu maswali yote, marahisi katika kutunga, yanarahisisha mwanafunzi kubuni jibu*, n.k. Miongoni mwao walikuwepo waliochanganya jibu sahihi na yasiyo sahihi, hivyo walipata alama hafifu. Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu hafifu katika swali hili.


10. (i) Kuangalia uelewa wa wanafunzi
(ii) Kufanya tathmini ya somo.
(iii) Kubaini ni ubinu au njia gani atakazo zitumia katika ufundishaji
(iv) Kutoa maelezo ya tathmini ya wanafunzi kwa wazazi au walezi.

**Kielelezo Na. 10.1:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuelewa matakwa ya swali.

Katika Kielelezo Na. 10.1 mtahiniwa alitaja faida ya zana za upimaji badala ya manufaa ya maswali ya kuchagua, hivyo alipata alama hafifu.

Kwa upande mwingine, asilimia 26.3 ya watahiniwa waliopata ufaulu mzuri katika swali hili, walikuwa na maarifa ya kutosha katika dhana nzima ya *zana za Upimaji katika somo la Uraia* na walielewa vyema matakwa ya swali. Watahiniwa hawa waliweza kutaja manufaa matatu au yote manne ya maswali ya kuchagua katika upimaji wa somo la Uraia. Baadhi ya hoja sahihi walizotoa ni kama vile; *huweza kupima sehemu kubwa ya maudhui kutokana na vichachawizi vilivyoandaliwa vizuri, huweza kupima maeneo mengi zaidi kwenye majazi ya utambuzi, ni rahisi kuyasahihisha na kutoa alama bila upendeleo*, n.k. Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali.




**Kielelezo Na. 10.2:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.

Katika Kielelezo Na. 10.2 mtahiniwa alitaja kwa ufasaha manufaa ya maswali ya kuchagua katika Upimaji wa somo la Uraia, hivyo alipata alama za juu.

Aidha, wengi wa watahiniwa waliopata kuanzia alama 2 hadi 2.5 katika swali hili, walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi, kwa mafano, mtahiniwa mmoja alichanganya hoja zisizo sahihi katika majibu yake kamavile: *Humsaidia kujua maswali ambayo yana changamoto*, *hukuza stadi ya ufahamu*. Wengine walitoa hoja pungufu, hivyo kushindwa kupata alama za juu.


## 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma)

Katika sehemu hii kila swali lilikuwa na jumla ya alama 15. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alikuwa na kiwango hafifu, wastani na kizuri cha ufaulu endapo alipata kuanzia alama 0 hadi 5.5, 6 hadi 10 na 10.5 hadi 15, mtawalia.

### 2.2.1 Swali la 11: Dola

Watahiniwa walitakiwa kufafanua kwa kutumia hoja tano umuhimu wa ushindani wa kidemokrasia katika siasa ya vyama vingi nchini Tanzania. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 2,871 sawa na asilimia 60 ya watahiniwa 4,787 waliofanya Mtihani wa somo la Uraia. Kati ya watahiniwa waliochagua kujibu swali hili, mtahiniwa mmoja sawa na asilimia 0.0 alipata alama 1, ambao ni ufaulu hafifu, watahiniwa 98 (3.4%)

walipata ufaulu wa wastani wa kuanzia alama 6 hadi 10 na watahiniwa 2,773 (96.6%) walipata ufaulu mzuri wa kuanzia alama 10.5 hadi 14.5. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa asilimia 100 ya watahiniwa waliweza kupata kuanzia alama 6 hadi 14.5 kama inavyoonekana katika Chati Na. 11.




**Chati Na. 11:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 11*

Watahiniwa 2,773 (96.6%) waliopata alama za juu katika swali hili waliweza kufafanua umuhimu wa ushindani wa kidemokrasia katika siasa ya vyama vingi nchini Tanzania kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua umuhimu wa ushindani wa kidemokrasia katika siasa ya vyama vingi nchini Tanzania kwa kutoa hoja kama vile: *Kukuza demokrasia nchini*, *kuchangia na kuhamasisha maendeleo ya wananchi*, *kutatua kero mbalimbali za wananchi*, *kufichua maovu na uvunjaji wa sheria unaofanywa na viongozi waliopo madarakani*, *kuhamasisha umoja, amani na utulivu nchini*, nk. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada nzima ya *Dola*, hasa kipengele cha *Utawala wa Kidemokrasia*, hivyo walitoa maelezo sahihi katika hoja zao. Kielelezo Na. 11 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri na kukidhi matakwa ya swali.


19 Demokrasia. Ni serikali ilichaguliwa na watu na ya watu ili itumike kuwaongoza watu. pia mfano wa vyama vingi Tanzania ulianzishwa mwa 1922 ikawa na lengo la kuwaidia raia kuwa kombo katiba malalamiko mbalimbali.

Ufuatao ni umuhimu wa ushindani wa kidemokrasia katika siasa ya yavyama vingi nchi Tanzania:-

Husaidia kuboresha miundo mbinu, kutokana na kuwepo kwa vyama vya ushindani kuweza kusaidi kuboresha miundo mbinu kuo kutoa misaada kutoka mashirika mbali mbali ya vyama vya kisiasa katika ushindani wakutaka kuwa viongozi katika nchi na kuweza kuwa na maboresho maalumu.

Husaidia kuleta maendeleo ya nchi; katika suala zima la ushindani wa vyama kuweza kusaidia katika uletaji wa maendeleo katika jamii kutokana na kuwa na mikakati ya vyama vyao katika nchi husaidia na kwa kupanga maboresho ya maendeleo kutokana na ushindani wa vyama vingi mfano ccm, Caffu, AIP na vinginevyo.

Husaidia kuondoa rushwa katika nchi; katika suala zima la ushindani wa vyama kuna baadhi ya vyama vina weza kuondoa rushwa mfano chama cha TANU enzi za nyerere kiliweza kupinga rusha kuanzia chama cha CCM kinasaidia suala zima la rushwa ambazo zinajitokeza bila mtu yeyote wowote we katika nchi yetu ambayo tunaishi na kushinikana zaidi kuanza


11: Husaidia kutatua kero za raia. katika suala zima la ushindani wa vyama vingi baadhi ya vyama vinafanya kazi ya kutatua kero ambazo zinajitokeza miongoni mwa raia katika jamii na kuweza kusaidia katika kufanya maboresho ambayo yanaweza kutokea katika nchi ambazo huwa tunaishi.

Husaidia kulinda haki za raia. kutokana na ushindani ambao unatokea katika nchi kuweza kusaidia baadhi ya vyama vinaweza kulinda haki zao katika jamii na kuweza kutatua matatizo ya wananchi kutokana na kuwepo kwa vyama vingi katika nchi ambayo vinaweza kusaidia katika kutatua kero ambazo zinazotokea katika jamii husika

Hivyo basi, katika suala zima la ushindani wa kidemokrasia katika siasa ya vyama vingi nchini Tanzania vimeweza kuleta faida pamoja na athari moja ya athari hii ni kupeleka uwajibikaji duni, rushwa kushindwa kutatua kero za raia, kushindwa kulinda haki za raia kutokana na baadhi ya vyama kutokuwa na mitaji ya kujiendesha kuweza kupeleka uwajibikaji kushindwa kufikia malengo ambayo wamekusudia katika jamii husika kwa ujumla kuweza kusaidia katika ongezeko la kuwepo kwa vyama hivyo katika nchi.

**Kielelezo Na. 11:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali.

Katika Kielelezo Na. 11 mtahiniwa alifafanua kwa usahihi umuhimu wa ushindani wa kidemokrasia katika siasa ya vyama vingi nchini Tanzania, hivyo alipata alama za juu.


Baadhi ya watahiniwa wachache (3.4%) waliopata kuanzia alama kati ya 6 hadi 10 katika swali hili, walidhihirisha kuwa na maarifa ya wastani juu ya dhana ya *Utawala wa Kidemokrasia*, hivyo walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya hoja kama vile: kila *raia ana haki ya kupiga kura, uhuru wa upigaji kura* na *ushriki katika kampeni*, bila ufafafanuzi wa hoja hizo, hivyo alipata alama pungufu.

Watahiniwa wengine walionesha kuwa na mapungufu mbalimbali katika insha zao, kama vile: utangulizi usiojitosheleza, kushindwa kutoa ufafanuzi wa kutosha kutetea hoja zao, kurudia hoja yenye maana moja na hitimisho lisilo na uhusiano na swali, hivyo walipata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hitimisho lifuatalo: *hivyo basi ni vyema kudumisha vyama kwa sababu huondoa ubaguzi katika jamii*. Katika hitimisho hili, mtahiniwa hakutoa maelezo ni vyama vipi au ubaguzi upi, hivyo alikosa alama za hitimisho.

Aidha, uchambuzi zaidi katika swali hili unaonesha kuwa mtahiniwa mmoja aliyepata alama 1 hakuwa na uelewa wa kina kuhusu mada ndogo ya *Utawala wa Kidemokrasia*, hivyo alishindwa kuandika majibu katika swali hili. Mtahiniwa aliandika utangulizi tu ambao, pia haukujitosheleza, hivyo alipata alama 1.

### 2.2.2 Swali la 12: Utamaduni wetu

Swali hil ililiwataka watahiniwa kuchambua athari tano za ukiukwaji wa haki za watoto ndani ya familia. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 3,715 sawa na asilimia 77.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani wa somo la Uraia. Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 6 (0.2%) walipata ufaulu hafifu wa kuanzia alama 2 hadi 5. Watahiniwa 198 (5.3%) walikuwa na ufaulu wa wastani wa kuanzia alama 6 hadi 10 na watahiniwa 3,511 (94.5%) walikuwa na ufaulu mzuri wa kuanzia alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa asilimia 99.8 ya watahiniwa waliweza kupata kuanzia alama 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na. 12.




**Chati Na. 12:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 12*


Watahiniwa waliopata kuanzia alama 10.5 hadi 15 waliweza kubaini matakwa ya swali na walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana nzima ya *Utamaduni Wetu*, hasa kipengele cha *Masuala kuhusu maisha ya familia*. Watahiniwa hawa waliweza kuchambua athari za ukiukwaji wa haki za watoto ndani ya familia kwa kutoa hoja kama vile: *kutokea kwa migogoro ndani ya familia*, *kukua kwa umaskini ndani ya familia*, *watoto kuathirika kisaikolojia hali inayoweza kupelekea kushuka kitaaluma shuleni*, *kupelekea ongezeko la watoto wa mitaani*, *kuongezeka kwa ndoa za utotoni*, *kuongezeka kwa magonjwa,* n.k. Ufaulu mzuri katika swali hili, umesababishwa na kuwa dhana ya haki za watoto huzungumzwa kwa mifano katika mazingira yao kuanzia ngazi ya familia hadi ya nchi. Aidha, tofauti za alama za watahiniwa katika kundi hili imetokana na kiwango cha usahihi wa maelezo katika hoja zao. Kielelezo Na. 12.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kutoa majibu sahihi katika swali hili.

12 Haki ni jumla ya mambo yote ambayo yanakubalika kisheria mtu kuyapata, kwa mujibu wa Sheria na Katiba ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania mtoto ni yule ambaye hajafikisha miaka 18, Hivyo haki za watoto ni yale mambo ambayo mtoto anapaswa kufanyiwa ambayo yanakubalika kisheria na jamii inayomzunguka. Zifuatazo ni athari tano za ukiukwaji wa haki za watoto ndani ya familia:-

Ongezeko la watoto wa mitaani, watoto wa mitaani ni watoto wasio na makazi maalumu huishi mitaani na hawana wa kuwasimamia, hivyo migogoro katika familia huongeza watoto wa mitaani.

Magonjwa ya Zinaa, kukiuka ni kufanya jambo kinyume na maridhiano yetu, mfano kumbaka mtoto, kumlawiti hali ambayo humpelekea mtoto kuambukiza wa baadhi ya magonjwa kama kaswende, kisonono na hata ukimwi

Vifo, kama ikitokea mtoto akilawitiwa na akahisi hioni kinyume na haki zake au akabakwa na jamii ikalitambua hilo humpelekea mtoto huyo kuwa na msongo wa mawazo na akikosa mtu wa kumshawishi vizuri huenda akachukua maamuzi magumu ya kujitoa uhai wake, jamii imeshuhudia matukio mengi sana ya aina hii.


12 Kuongezeka kwa makundi ya kihalifu, mfano-
hapa Tanzania kuna kipindi kundi la kihalifu la pa-
nya road lilishamiri sana kwa kufanya uhalifu, sio hivyo
tu pia yameshajitokeza makundi kadhaa ya watoto kama
watoto wa mbwa, Uswahilax na mengineye ya kihalifu-
kwa minadhiri ya kupindua nchi.
Migogoro ya kifamilia, huenda haki za mtoto ni-
baba au mama hazitimizi hali hii husababisha migogo-
ro mikubwa sana ya kifamilia ambayo hupelekea maha-
kani kujaa kesi nyingi za kifamilia, hivyo haki za wato-
to zikikiukwa hutokea migogoro mingi sana ya kifamilia.
Kwa ujumla ukiukwaji wa haki za binadamu -
hudumaza ustawi wa jamii, haki za binadamu zina uhusi-
ano wa moja kwa moja na haki za watoto hivyo ukiuk-
waji huu husababisha ustawi mdogo wa jamii.


**Kielelezo Na. 12.1:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.

Katika Kilelezo Na. 12.1 mtahiniwa alichambua kwa usahihi athari za ukiukwaji wa haki za watoto ndani ya familia, hivyo alipata ufaulu mzuri.

Kati ya asilimia 5.3 ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 6 hadi 10, walishindwa kutoa maelezo sahihi kutetea baadhi ya hoja zao na wengine walitoa hoja pungufu ya tano zilizohitajika kwenye swali. Miongoni mwao walikuwepo walioshindwa kutoa utangulizi na hitimisho lenye uhusiano wa moja kwa moja na swali. Hali kadhalika, wengine walikosa maarifa juu ya mpango mzuri wa uandishi wa insha, hivyo walipata alama za wastani.

Aidha, baadhi ya watahiniwa 6 waliopata kuanzia alama 2 hadi 5, hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana ya *Masuala kuhusu maisha ya familia*, hivyo walitoa hoja zisizo na uhusiano wa moja kwa moja na swali. Wengine hawakuelewa vyema matakwa ya swali, hivyo walitoa majibu kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja


alichambua sababu za vitendo vya ukiukwaji wa haki za watoto ndani ya familia badala ya athari za ukiukwaji wa haki za watoto ndani ya familia kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 12.2.


12. Ukiukwaji wa haki za watoto. Ni kwenda kinyume na taratibu, sheria na kanuni za familia, kwa kufanya kitu chochote anachofikiria bila kujali kina faida au madhara.
Zifuatazo ni athari za ukiukwaji wa haki za watoto ndani ya familia:
Ukosefu wa elimu, kutokana na elimu ndogo walizonazo watu katika familia husababisha kwenda kinyume na haki za watoto, ~~kama~~ watoto hawapatiwi haki zao.
Ukosefu wa mahitaji ya msingi. Kutokana na ukosefu wa mahitaji ya msingi ambao unasababishwa na hali duni ya maisha husababisha famili kwenda kinyume na haki za watoto kwa kutowapatia mahitaji kama chakula, malazi, upendo, mavazi.
Kutokuwepo kwa vyombo vya haki za binadamu, ambavyo vinasaidia kutetea haki za binadamu husababisha familia kwenda kinyume na haki za watoto.
Ubaguzi. haki za watoto hukiukwa kutokana na ubaguzi wa watoto kwa kupendelea jinsi moja kwa kuwapatia mahitaji na wengine kutowapatia mahitaji.
Hivyo! Ukiukwaji wa haki za watoto ndani ya familia huweza kusababisha watoto kupata mimba kutokana na ukosefu wa mahitaji yao ya msingi, watoto wa mitaani, husababisha vifo pamoja na magonjwa.

**Kielelezo Na. 12.2:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeenda kinyume na matakwa ya swali.

### 2.2.3 Swali la 13: Uchumi wa Tanzania

Swali hili liliwataka watahiniwa, kwa kutumia hoja sita, kueleza namna Tanzania inavyonufaika na uchumi wa soko huria. Kati ya watahiniwa 2,985 waliochagua kufanya swali hili, watahiniwa 102 (3.4%) walikuwa na ufaulu hafifu wa kuanzia alama 0 hadi 5.5. Watahiniwa 1,933 (64.8%) walipata ufaulu wa wastani wa kuanzia alama 06 hadi 10 na watahiniwa 1,531 (31.8%) walipata ufaulu mzuri wa kuanzia alama 10.5 hadi 14. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa asilimia 96.6 ya watahiniwa waliweza kupata alama 2 hadi 4 ambao ni ufaulu wa wastani hadi mzuri kama inavyoonekana katika Chati Na. 13.




**Chati Na. 13:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 13*

Baadhi ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 6 hadi 10 katika swali hili, walishindwa kutoa maelezo sahihi katika kutetea baadhi ya hoja zao ambapo wengine walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho lililojitosheleza. Miongoni mwao wapo waliochanganya hoja sahihi na zisizo sahihi, hivyo kuwafanya wapate alama pungufu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja ambazo si sahihi kwenye majibu yake kama vile; *uwajibikaji* na *uzalendo* bila maelezo yenye kuziunganisha na faida za soko huria kwa Tanzania, hivyo kumfanya apate alama za wastani.

Watahiniwa waliopata kuanzia alama 10.5 hadi 14 walielewa vyema matakwa ya swali na waliweza kueleza namna Tanzania inavyofaidika na uchumi wa soko huria. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kina kuhusu mada ndogo ya *Uchumi wa Soko Huria*. Baadhi ya majibu sahihi katika swali hili ni kama ifuatavyo: *Upatikanaji wa bidhaa mbalimbali kwa wingi na zenye ubora, kuwepo kwa ushindani wa kibiashara kwa wazalishaji mbalimbali, umechangia ongezeko la ajira na kukua kwa sekta isiyo rasmi, uchumi wa soko huria umesaidia serikali kuongeza wigo na pato la nchi linalotokana na wafanyabiashara kulipa kodi,* n.k. Kielelezo Na. 13.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.

13 Soko huria ni Kitendo cha Kununua na Kuuza bidhaa Kutoka nje za nchi. Mfano unaweza Kupeleka bidhaa zako nchi jirani Kenya bila Kuzuiliwa na ukanunua bidhaa zako. faida ya soko huria Tanzania ni

Kupanua soko la bidhaa za Tanzania nje za nchi. Katika soko huria tunafaidika kwa Kuitangaza bidhaa zetu katika nchi nyingine na Kupata wateja. Mfano Madini ya Tanzanaiti tuna uza katika nchi nyingine sababu kuna soko huria.

Tunapata fedha za Kigeni; Nchi nyingine zinapokuja kufanya biashara katika nchi ya Tanzania kutumia fedha zao kununua bidhaa Mfano Tunapouza madini tunauza kwa mfumo wa dola hivyo tunajipatia fedha za kigeni ni faida ya soko huria.

Tunajenga urafiki na nchi jirani duniani Tunapofanya biashara, tunajenga urafiki na nchi ambayo tunaiuzia bidhaa au inayoleta bidhaa nchi Mfano Tanzania na China ni marafiki wa Kibiashara sababu ya soko huria tunakuwa Marafiki na ~~cha~~ nchi nyingine duniani.

Tunaongeza pato la taifa. Wafanyabiashara wanaponunua bidhaa zetu wanalipia kodi zile bidhaa kodi hiyo ni pato la taifa ambalo kutumika katika shughuli nyingine Mfano tunatumia kujenga shule, hospitali, na Miundombinu mbalimbali nchi Tanzania

Chanjo cha ajira kwa Watanzania: Tunago tumia soko huria watanzania kujipati ajira ya kusafirisha mzigo kujifanyia biashara katika nchi nyingine Kununua bidhaa na kuleta

13 nchini Tanzania Mfano Katika uwekezaji wa ma
dini watanzania kupata ajira ya kuchimba ma
dini na kuyauza katika nchi nyingine ni
faida ya soko huria.


Uchumi wa nchi unaendelea kukua kwa
kiwango kikubwa; tunapo uza bidhaa nje za
nchi bei yake kuwa juu ambayo kuleta faidi
katika kukua kwa uchumia nchini Tanzania
Mfano; Tunapouza madini katika nchi za ulaya
tunauza kwa bei kubwa ili tupate faida ndipo
uchumi unakua.

Hizi ni faida za soko huria japo kuna
athari nyingi katika mfumo huu wa soko
huria Mfano; kuenea kwa magonjwa, kuporomo
ka kwa madili, ajari kuweza kutokea ni ma
dhara ya soko huria katika nchi ya Tanzania.

**Kielelezo Na. 13.1:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali.

Katika Kielelezo Na. 13.1 mtahiniwa alieleza kwa usahihi namna Tanzania inavyonufaika na uchumi wa soko huria, hivyo alipata ufaulu mzuri.

Watahiniwa waliopata kuanzia alama 0 hadi 5.5 walishindwa kutambua matakwa ya swali. Wengi wao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana ya *uchumi wa soko huria*. Wengine walichanganya maarifa na kueleza hoja ambazo hazina uhusiano kabisa na matakwa ya swali. Mtahiniwa mmoja miongoni mwao alitoa hoja ambazo hazina uhusiano na uchumi wa soko huria. Kwa mfano, hoja za *usawa*, *utawala wa huru na haki, uhuru* na *haki za binadamu* ambazo ni dhana mbalimbali katika somo la Uraia kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 13.2.



13. Uchumi wa soko huria:- Hii ni ile haki ya binadamu au mlaji kuwa na uwezo wa kununua bidhaa popote atakapo. Zifuatazo ni namna Tanzania inavyofaidika na uchumi wa soko huria:-

Usawa:- Hii ni namna ya kwanza ambayo Tanzania inafaidika na uchumi wa soko huria kwa sababu kila binadamu ana haki sawa na mwenzake ya kuuza au kununua bidhaa popote anapotaka yeye mwenyewe bila kujali ukubwa, kabila wala rangi ya mtu huyo.

Utawala wa huru na haki:- Pia hii ni namna nyingine ambayo Tanzania inafaidika na uchumi wa soko huria kutokana na kuwepo na utawala ulioko huru na wa haki kwa mtu yoyote kufanya biashara mahali popote anavyotaka na kuweza kupata uhuru wake pamoja na haki zake.

Haki za binadamu:- Pia hii ni namna nyingine Tanzania inavyofaidika na uchumi wa soko huria kwa sababu uchumi huu umekuwa ukizingatia binadamu kuwa na haki zake zote za msingi ambazo binadamu huyo anapaswa kuzipata na ndio maana tunasema kwamba uchumi wa soko huria unafanya Tanzania kuweza kufaidika.

Uhuru:- Pia hii ni namna Tanzania inavyofaidika na uchumi wa soko huria kwa sababu ni haki ya mlaji kufanya biashara mahali popote atakapo pia ni haki ya kila mtu kuweza kununua bidhaa mahali


**Kielelezo Na. 13.2:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu hafifu.

## 2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha (Utaalamu)

Katika sehemu hii, kila swali lilikuwa na jumla ya alama 15. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu. Mtahiniwa alikuwa na kiwango hafifu, wastani na kiwango kizuri cha ufaulu endapo alipata kuanzia alama 0 hadi 5.5, 6 hadi 10 na 10.5 hadi 15, mtawalia.

### 2.3.1 Swali la 14: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Uraia


Swali hili liliwataka watahiniwa kueleza mambo matano ya kuzingatia wakati wa kufundisha stadi katika somo la Uraia. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 3,035 (63.4%) kati ya watahiniwa 4,787 (100%) waliofanya mtihani wa somo la Uraia. Kati ya watahiniwa waliofanya swali hili, watahiniwa 2,547 (83.9%) walipata ufaulu hafifu wa kuanzia alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 379 (12.5%) walipata ufaulu wa wastani wa kuanzia alama 6 hadi 10 na watahiniwa 109 (3.6%) walipata ufaulu mzuri wa kuanzia alama 10.5 hadi 14.5. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kuwa ni asilimia 16.1 tu ya watahiniwa ndio waliweza kupata alama 6 hadi 14.5. Chati Na. 14 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 14:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 14*

Asilimia 83.9 ya watahiniwa waliopata alama hafifu walishindwa kueleza kwa usahihi mambo ya kuzingatia wakati wa kufundisha stadi katika somo la Uraia. Baadhi yao walishindwa kutoa utangulizi uliojitosheleza, maelezo

ya kina kutetea hoja zao na hitimisho lenye uhusiano na hoja. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile: *utulivu wa wanafunzi*, *uelewa wa wanafunz*i, *jinsi ya kulitawala darasa na utulivu wa darasa* ambazo hazikuwa na maelezo yenye kujitosheleza, hivyo alipata alama hafifu. Wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali, hivyo walitoa hoja zilizo nje ya swali zilizopelekea kupata alama 0. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua hoja kama vile; kujiamiini, uthubutu, mawasiliano, ushirikiano, mwaminifu, n.k., kama inavyoonekana katika Kilelezo Na. 14.1.




**Kielelezo Na. 14.1:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.

Katika Kielelezo Na. 14. 1 mtahiniwa alijaribu kutaja sifa za mwalimu anayefundisha stadi za Uraia badala ya mambo ya kuzingatia wakati wa kufundisha stadi katika somo la Uraia.

Kwa upande mwengine, asilimia 12.5 ya watahiniwa walitoa hoja pungufu pamoja na maelezo yasiyokuwa na mifano. Pia, baadhi yao walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho lilijitosheleza, hivyo walipata alama za wastani (6 hadi 10). Wengine kati yao, walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi katika insha zao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya hoja kama vile; *mwanafunzi aweze kutambua misingi ya demokrasia*, *mwanafunzi aweze kutambua umuhimu wa katiba*, ambazo hazikuwa sahihi, hivyo kumsababishia kupata alama pungufu.

Aidha, watahiniwa waliopata alama 10.5 hadi 14.5 waliweza kueleza kwa ufasaha mambo ya kuzingatia wakati wa kufundisha stadi katika somo la Uraia. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ndogo ya *Ufundishaji unaozingatia ujenzi wa stadi na ujuzi wa Kiraia*, na walielewa vema matakwa ya swali. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa katika swali hili yalikuwa kama ifuatavyo: *Stadi yeyote hupatikana kutokana na mazoezi yanayorudiwarudiwa, stadi hutokana na vitendo atakavyofanya mwanafunzi kwa kufikiri na kutenda, mwalimu anapoandaa somo ahakikishe anampatia mwanafunzi motisha ya kupenda kujifunza zaidi stadi inayohusika, mwalimu anapaswa kuwapa wanafunzi wake nafasi ya kuelezea matumizi na manufaa ya stadi wanazojifunza, wanafunzi wanahitaji kupewa nafasi ya kutafuta, kuchambua na kutumia taarifa hizo katika kujadili masuala ya kijamii na kisiasa, n.k.* Kielelezo Na. 14.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa moja aliyeweza kueleza kwa ufasaha mambo matano ya kuzingatia wakati wa kufundisha stadi katika somo la Uraia.

14. stadi; ni ujuzi wa kufanya jambo fulani kama vile kufikiri na kutumia stadi ndogondogo kupanga na kuongoza. yafuatayo ni mambo ya kuzingatia wakati wa kufundisha stadi katika somo la Uraia:-

Kuwapa wanafunzi mazoezi ya kujiendiandia; stadi hujengwa kwa mazoezi ya kujiendiandia. Hivyo ni vyema mwalimu ahimize wanafunzi kufanya mazoezi mengi.

Wanafunzi watumie vitendo vya kufikiri na kutenda; ili wanafunzi waweze kufikiri na kutenda wapewe kazi zinazochochea udadisi pamoja na ubunifu.

kutoa motisha ya kujifunza kwa wanafunzi; motisha ni kichocheo kinachofanya mwanafunzi apende kujifunza. kwa mfano kuwashirikisha katika kuamua jambo na kutobagua jinsia wakati wa ufundishaji.

Kuwapa wanafunzi nafasi ya kuelezea manufaa ya walichojifunza katika kipindi. Mwanafunzi atambue umuhimu wa kile alichojifunza darasani mfano kuhusianisha somo na maisha yake ya kila siku.


Kuwapa muda wa kutafuta kuchambua na kutumia taarifa; taarifa hizo wanaweza kuzipata kupitia vyombo vya habari. Hivyo mwalimu anatakiwa kuwajengea stadi ya kutafuta, kuchambua na kuzitumia taarifa walizozipata.

Hivyo basi Mwalimu anapaswa kutumia mbinu mbalimbali kwa mfano kulinganisha maarifa waliyonayo wanafunzi na anachofundisha ili kuwajengea kumbukumbu za stadi wanazojifunza.

**Kielelezo Na. 14.2:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa jibu sahihi katika swali hili.

### 2.3.2 Swali 1a 15: Zana za kufundishia na Kujifunzia

Swali hili liliwataka watahiniwa kuchambua mambo sita muhimu ya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana za kufundishia. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,779 (99.8%) ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Watahiniwa 129 (2.7%) walipata ufaulu hafifu wa kuanzia alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 3,185 (66.6%) walipata ufaulu wa wastani wa kuanzia alama 6 hadi 10 na watahiniwa 1,465 (30.7%) walipata ufaulu mzuri wa kuanzia alama 10.5 hadi 14. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili ni kizuri kwa kuwa asilimia 97.3 waliweza kupata kuanzia alama 6 hadi 14. Chati Na. 15 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 15:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 15*

Asilimia 66.6 ya wataniniwa walipata alama za wastani kwa sababu baadhi yao walishindwa kufafanua hoja kwa usahihi na walitoa hoja pungufu. Wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya sifa za zana za kufundishia na kujifunzia kwa hoja kama vile: *ichochee udadisi*, *imjengee mwanafunzi uelewa*, *isiwe hatarishi* ambazo hazikuwa sahihi kulingana na matakwa ya swali. Aidha, baadhi ya watahiniwa licha ya kuwa na dosari mbalimbali, pia walishindwa kutoa maelezo sahihi katika sehemu ya utangulizi na hitimisho, hivyo walipata alama pungufu.

Watahiniwa waliopata kuanzia alama 10.5 hadi 14 waliweza kuchambua mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia katika somo la Uraia. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ndogo ya *Matumizi na utunzaji wa zana za kufundishia na kujifunzia* na waliweza kwa usahihi kutambua matakwa ya swali. Baadhi ya majibu sahihi katika swali hili yalikuwa kama ifuatavyo: *kutokung'ang'ania aina moja ya vifaa au malighafi katika kutengeneza zana*, *kushirikisha wanafunzi na wakati mwingine jamii husika ili walete malighafi zinazopatikana katika mazingira yao*, *kuhakikisha zana zinakidhi malengo ya mada inayokwenda kufundishwa pamoja na kuzingatia umri na idadi ya wanafunzi*, *kuzingatia uhalisia wa zana kwa kile kitakacho fundishwa*, n.k. Kielelezo Na. 15.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

15 Zana kendane na idadi ya walengwa; Mwalimu anapotengeneza zana za kufundishia atengeneze nyingi na za kutosha ili kuendana na idadi ya wanafunzi anaoenda kuwafundisha.

Upatikanaji rahisi wa malighafi ya bei nafuu; Wakati mwalimu anapotengeneza zana kwa kutumia malighafi halisi ahakikishe yanapatikana kwa urahisi na hayaitaji gharama kubwa ili mwalimu kutengeneza pamoja na wanafunzi.

Ushirikishwaji wa wanafunzi pamoja na jamii; Wakati mwalimu anapotengeneza zana awashirikishe wanafunzi hatua kwa hatua ili kila mwanafunzi awe na zana yake pia anapoenda nyumbani ni rahisi yeye kutengeneza na kukuza ubunifu.


Ujuzi binafsi wa mwalimu; Wakati mwalimu anapotengeneza zana ahakikishe kuwa ana ujuzi wa kile anachokitengeneza ili aweze kumfikirisha mwanafunzi kama anaona hawezi ni vizuri kuomba msaada kwa mwalimu mwenzake ili aweze kutengenezewa zana yenye ubora.

∴ Hivyo basi, Kutengeneza zana ni muhimu sana kwa kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji na pia unatumia malighafi halisi yanayopatikana katika mazingira. Hivyo wizara ya elimu itoe elimu kwa walimu mashuleni umuhimu wa mwalimu kufundisha kwa kutumia zana kama vile kumjengea mwanafunzi kumbukumbu ya muda mrefu kuibua udadisi na

**Kielelezo Na. 15.1:** Sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa.

Katika Kielelezo Na. 15.1 mtahiniwa alichambua kwa usahihi mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana za kufundishia, hivyo alipata ufaulu mzuri.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa wachache (2.7%) waliopata kuanzia alama 0 hadi 5.5, walishindwa kukidhi matakwa ya swali na wengine walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika dhana nzima ya *Matumizi ya zana*. Aidha, wapo waliochanganya maarifa na kutoa majibu kinyume na swali lilivyouliza, hivyo kusababisha kupata alama 0. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zinazoonesha hatua za kuzingatia katika kutengeneza zana kama vile; *matayarisho*, *maandalizi*, *maamuzi*, *matengenezo*, *marekebisho* au *maboresho* na *matumizi*. Mtahiniwa mwingine alichambua hatua na mahitaji ya kuzingatia katika kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia badala ya mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia. Alifaya hivyo kwa kutoa hoja kama vile: *wazo la kutengeneza*, *ujuzi wa kutengeneza*, *ubora wa vifaa vya kutengenezea zana*, *ujuzi wa kutumia zana*, *n.k.*, kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 15.2.


15 Kutengeneza, ni kitendo cha kuunda zana bora kwaajili ya kufundishia ya kujifunzia somo husika. hivyo basi kuna vitu ambavyo mwalimu anatakiwa kuwanavyo makini au kuzingatia wakati au pindi anapotakiwa kutengeneza zana yake:-

Wazo la kutengeneza, Mwalimu lazima awe na wazo la kutengeneza zana zake, ili aweze kufikia kile anachohitaji lazima awe na wazo ambalo lina weza kumwezesha kutengeneza zana yake na kuweza kuwa imara na yenye mvuto katika darasa na yenye kuwe ndana na somo husika.

Kuwa na vifaa au vitu vya kutengenezea inatakiwa Mwalimu awe kuwa na vifaa ambavyo vitamwezesha yeye kutengeneza na kuweza kufikia lengo la ufundishaji na ujifunzaji kufika na hali halisi ambayo inatakiwa katika suala zima la ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo.


Ujuzi wa kutengeneza, inatakiwa Mwalimu awe na ujuzi juu ya kutengeneza zana hiyo na kuweza kufikia pale ambapo alitarajia kufika kwa muda husika kuweza kurahisisha mambo kuwa katika hali ya kufikia lengo na kufanya mazoezi kwenye somo husika na mada ambayo imefundishwa.

**Kielelezo Na. 15.2:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu hafifu.

### 2.3.3 Swali la 16: Upimaji na Tathmini

Swali hili liliwataka watahiniwa kufafanua misingi sita ya kufuata wakati wa kufanya tathmini katika somo la Uraia. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,719 (36%). Watahiniwa 1,620 (94.2%) walipata ufaulu hafifu wa kuanzia alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 65 (3.8%) walipata ufaulu wa

wastani wa kuanzia alama 6 hadi 10 na watahiniwa 34 (2%) walikuwa na ufaulu mzuri wa kuanzia alama 11 hadi 14. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kuwa ni asilimia 5.8 tu ya watahiniwa ndio waliweza kupata kuanzia alama 6 hadi 14 kama inavyoonekana katika Chati Na. 16.




**Chati Na. 16:** *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 16*

Asilimia 94.2 ya watahiniwa walipata alama hafifu katika swali hili. Baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo walitoa majibu yasiyo na uhusiano na kilichoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua dhana mbalimbali zinazofundishwa katika mada ya *Misingi ya Ufundishaji wa somo la Uraia* kwa hoja kama vile: *uhusishi wa raia na bunge la Jamhuri ya Muungano*, *uhusishi wa dhana tata*, *masuala chanya na hasi ya kisiasa na kiserikali*, *utekelezaji wa haki na wajibu*, hivyo alipata alama 0. Watahiniwa wengine walidhihirisha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Upimaji na Tathmini*, hasa kipengele cha *Tathmini* katika somo la Uraia, hivyo walitoa hoja dhaifu zilizosababisha kupata ufaulu hafifu. Kati yao, walikuwepo walioshindwa kutoa utangulizi na hitimisho lenye uhusiano na swali. Kielelezo Na. 16.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.

16 Uraia ni somo linahusu haki za binadamu na wajibu wa raia katika nchi ifuatayo ni Misingi ya kuzingatia wakati wa kufanya tathmini katika somo la uraia

Misingi inayozingatia changamoto na mafanikio ya haki za binadamu, Ni Msingi moja wapo ambao inataki wa uweze kufanyiwa tathmini katika somo la uraia

Misingi inayozingatia Maadili katika somo la uraia, Ni kweli kwa kufanya tathmini pia ya misingi hii tunaweza kugundua kwamba wapi maadili yanapoelekea na kuweza kutoa ushauri.

Misingi ya ufundishaji na ~~ufunzaji~~ ujifunzaji wa stadi za maisha, unafanya tathmini katika somo la uraia lazima uzingatie stadi za kuweza kuishi

16. na watu mbalimbali katika jamii ambayo inazunguka.

Misingi inayozingatia ufuataji wa katiba na vipengele vyake, Ni msingi muhimu moja wapo katika somo la uraia ambao ni vizuri kufanyiwa tathmini ili kuweza kubaini changamoto na mafanikio

Misingi inayozingatia utawala bora katika somo la uraia, Misingi inayozingatia kujifunza na kufundisha Misingi ya utawala bora katika somo la uraia na maadili

Misingi inayozingatia kuhimiza wajibu wa kila raia, katika somo la uraia kuna misingi ambayo huweza kuhimiza wajibu wa kila raia katika ujenzi wa nchi yake.

Hivyo basi, kulingana na maelezo ambayo ni moyaelezea kujifunza somo na Misingi ya uraia husaidia katika kudumisha upendo na amani

**Kielelezo Na. 16.1:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.

Katika Kielelezo Na. 16.1 mtahiniwa alitoa majibu ya kubuni kwa kuunganisha na mada mbalimbali zinazofundishwa katika somo la Uraia, hivyo alipata ufaulu hafifu.

Aidha, asilimia 3.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata ufaulu wa wastani kutokana na dosari mablimbali zilizobainika katika majibu yao kama vile: ufafanuzi dhaifu wa hoja, utoaji wa hoja pungufu ya idadi iliyotakiwa kwenye swali, utangulizi na hitimisho lisilo na uhusiano mzuri na swali na kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya hoja zisizo sahihi katika jibu lake kama ifuatavyo: *kuzingatia namna ya umaliziaji wa somo*, *kuzingatia ufundishaji*, hivyo alipata alama pungufu.

Watahiniwa waliopata alama 11 hadi 14 katika swali hili walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana nzima ya *Tathmini katika somo la Uraia* na walielewa vema matakwa ya swali. Watahiniwa hao waliweza kufafanua dhana ya tathmini na misingi ya kuzingatia wakati wa kufanya tathmini. Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa katika swali hili ni kama ifuuatavyo: *Kuhakikisha unaelewa kile unachokusudia kukifanyia tathmini*, *kuchagua njia/zana sahihi katika kufanya tathmini*, *kuelewa vikwazo vya njia utakayoitumia*, *kuelewa kuwa kila njia ya tathmini ina vikwazo vyake*, n.k. Uchambuzi zaidi umeonesha kuwa watahiniwa hawa waliweza kufanya vizuri kwa sababu mada ya *Tathmini na Upimaji* inafundishwa katika masomo mengi wanayojifunza, hivyo hii ilidhihirisha uwezo wao wa kuhawilisha maarifa waliyoyapata katika masomo mengine. Kielelezo Na. 16.2 kinaonesha sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.


16. Tathimini; Ni kitendo cha kukusanya data, kuichambua data na kufahamu mwanafunzi ameelewa kwa kiasi gani. Ili kufanya maamuzi sahihi ya data hizo ifuatayo ni miongozi ya kufuata wakati wa kutathimini somo la uraia nitaelezea kama ifuatavyo:-

Inatakiwa kuelewa kwa kina kile kinachotakiwa kufanyiwa tathimini kabla ya somo la uraia, mfano kutathimini wanafunzi walivyofanya vizuri katika kipengele flani katika somo la uraia mfano kutathimini matokeo ya wanachuo cha ualimu tandala katika kuweza kujieleza kwa ufanisi.

Kuwa na njia sahihi za kufanyia tathimini; katika tathimini ni lazima kuwa na njia sahihi ambazo zitawezesha katika kufanikisha shughuli nzima ya tathimini katika somo la uraia. Mfano wa njia hizo ni data za upimaji.

Kufahamu vikwazo mbalimbali; Mfano mwanafunzi anaweza kufeli mtihani kutokana na kutohudhulia vipindi darasani, na vivo kila mwanafunzi anaefeli darasani anauelewa mdogo pia zipo sababu za kumfanya afeli tofauti na uelewa mdogo.

Kuwa na zana sahihi za kufanyia tathimini; Mfano mitihani, majaribio, mazoezi mbalimbali na vivo kifaa kinachotumika kupimia mwendokasi wa


16 upepo kutumika kupimia uelewa wa wanafu
nzi hivyo katika kufanya tathmini ni lazima
mbinu kuwa na zana sahihi.
Kuelewa kuwa lengo la kufanya
tathmini ni kuboresha, Mfano kuboresha
zana za kufundishia, mbinu na njia
za kufundishia kuboresha mfumo
mzima wa elimu kwa kubadilisha
Mtaala mzima, katika somo la uraia
ambalo hufundishwa katika shule za
Msingi.
Inatakiwa misingi ya upimaji izingatiwe
katika kutathmini somo la uraia; mfano
upimaji uwe umegusa nyanja zote za
kielimu, upimaji uonekane kwamba kinachotakiwa
kupimwa, upimaji uzingatie
sehemu zote katika muhtasari, na uzi-
ngatie mazingira rafiki kwa mwanafunzi.
Kiujumla tathmini ina umuhimu
katika elimu mfano husaidia katika
kutoa vyeti, husaidia kufanya uteuzi
wa wanafunzi katika kuendelea na
masomo ya juu pia tathmini husaidia
kujua kama nguvu, jitihada hazijaenda
bure.

**Kielelezo Na. 16.2:** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali.

Katika Kielelezo Na. 16.2 mtahiniwa alifafanua kwa ufasaha misingi ya kufuata wakati wa kufanya tathmini katika somo la Uraia, hivyo alipata ufaulu mzuri.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Mtihani wa Uraia ulikuwa na maswali 16 yaliyotungwa kutoka kwenye mada 9 katika Muhtasari wa somo hili. Mada nne zilitoka upande wa Taaluma na mada tano upande wa Utaalamu/Ufundishaji. Kiwango cha

kufaulu katika mada zilizotahiniwa mwaka 2019 kilikuwa kizuri kwa sababu kati ya mada 9 zilizotahiniwa, watahiniwa walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu katika mada sita, wastani katika mada mbili na kiwango hafifu katika mada moja. Mada zilizokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu ni mada ya *Maandalizi ya Kufundisha somo la Uraia* iliyoongoza kwa kuwa na ufaulu wa asilimia 99.6, ikifuatiwa na *Utamaduni wetu* (99.5%), *Uchumi wa Tanzania* (96.6%), *Uhusiano wa Kimataifa* (93.7%), *Zana za Kufundishia na Kujifunzia* (92.5%) na mada ya *Dola* iliyokuwa na ufaulu wa asilimia 78.2.

Mada zilizokuwa na ufaulu wa kiwango cha wastani ni *Misingi ya Ufundishaji wa somo la Uraia* kwa asilimia 48.2 na *Uchambuzi wa Machapisho/Maandiko muhimu ya Kufundishia Somo la Uraia* asilimia 46.5. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa, watahiniwa walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu katika mada ya *Upimaji na Tathmini* iliyokuwa na asilimia 26.2 (Angalia kiambatisho).

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa wengi waliweza kufanya vizuri katika mada nyingi zilizotahiniwa kutokana na kuwa na ujuzi na weledi wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa walishindwa kufanya vizuri, hasa katika mada ya Upimaji na Tathmini. Baadhi ya sababu zilizopelekea kushindwa kwao ni kama ifuatavyo: Kuwa na uelewa mdogo katika kubaini matakwa ya swali, uelewa mdogo wa dhana nzima ya *zana za Upimaji* na dhana ya *Tathmini katika somo la Uraia*, ufinyu wa maarifa ya kuhawilisha taaluma/maarifa kutoka somo moja kwenda jengine; kwa kuwa mada ya *Upimaji na Tathmini* hufundishwa katika masomo mengi ya kozi ya Ualimu na uwezo mdogo wa kufafanua hoja kwa kutumia mifano, hasa katika maswali ya insha.

## 4.0 HITIMISHO

Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika Mtihani wa 612 Uraia 2019 kwa ujumla ni kizuri, kwa kuwa asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya Mtihani walipata asilimia 40 au zaidi. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada zilizotahiniwa, uelewa mzuri wa maswali mbalimbali yaliyoulizwa na uwezo mzuri wa kupanga kazi na kufafanua hoja mbalimbali. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa zipo changamoto mbalimbali za watahiniwa wachache walioshindwa kupata

alama za juu kama; uelewa mdogo wa matakwa ya swali, uwezo mdogo wa kujibu maswali, kushindwa kuhawilisha maarifa, kutofuata maelekezo, kushindwa kutoa ufafanuzi wa dhana walizoulizwa kwa usahihi na kukosa maarifa ya kutosha kuhusiana na dhana zilizoulizwa.

Taarifa hii itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Uraia kwani itatoa msingi kwa wakufunzi na wawezeshaji katika ufundishaji wa mada iliyoonekana kuwa na matatizo. Aidha, taarifa hii itatoa chachu kwa wanachuo na kuwahamasisha katika ujifunzaji wa mada zote za Taaluma na Utaalamu (ufundishaji) zilizopo katika muhtasari wa somo la Uraia.

Mwisho, taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa iwe msingi katika kuwasaidia wakufunzi na wanachuo kuyaelewa makosa yanayosababisha watahiniwa wachache kutojibu vizuri maswali na kisha kurekebisha kasoro zilizojitokeza. Aidha, taarifa hii itakuwa na tija kwa wakufunzi katika ufundishaji na upimaji, hivyo itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu katika somo hili.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanachuo inapendekezwa kuwa:

(a) Wakufunzi wa somo wajenge tabia ya kutoa mitihani, mazoezi na majaribio ya mara kwa mara ili kuwajengea walimu tarajali uwezo wa kujibu maswali kulingana na matakwa.

(b) Wakufunzi wanapaswa kufundisha kwa usahihi mada zote kama zilivyoainishwa kwenye Muhtasari wa somo hili ili kuwafanya walimu tarajali kuwa mahiri katika mada zote, hasa mada ya Upimaji na Tathmini.

(c) Walimu tarajali wahimizwe kusoma vitabu, makala na machapisho mbalimbali yanayohusu mada za somo la Uraia na masuala mtambuka ili kuongeza uelewa na maarifa wa dhana mbalimbali za somo hili.

(d) Wakufunzi wahimizwe kutoa mrejesho wenye kutatua changamoto zote za walimu tarajali katika uhawilishaji wa maarifa na ujibuji sahihi wa maswali ya insha mara baada ya majaraibio au mitihani ya mihula.

**Kiambatisho**

**UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA**

| Na. | Mada | Namba ya Swali | Asilimia ya Ufaulu | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliopata asilimia 40 na zaidi | Wastani | |
| 1 | Maandalizi ya kufundisha somo la Uraia | 9 | 99.6 | 99.6 | Vizuri |
| 2 | Utamaduni Wetu | 5 | 99.1 | 99.5 | Vizuri |
| | | 12 | 99.8 | | |
| 3 | Uchumi wa Tanzania | 13 | 96.6 | 96.6 | Vizuri |
| 4 | Uhusiano wa Kimataifa | 7 | 93.7 | 93.7 | Vizuri |
| 5 | Zana za Kufundishia na Kujifunzia | 6 | 87.6 | 92.5 | Vizuri |
| | | 15 | 97.3 | | |
| 6 | Dola | 1 | 99.1 | 78.2 | Vizuri |
| | | 3 | 35.4 | | |
| | | 11 | 100 | | |
| 7 | Misingi ya Ufundishaji wa somo la Uraia | 2 | 80.3 | 48.2 | Wastani |
| | | 14 | 16.1 | | |
| 8 | Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho muhimu ya kufundishia na kujifunzia somo la Uraia | 4 | 2.2 | 46.5 | Wastani |
| | | 8 | 90.7 | | |
| 9 | Upimaji na Tathmini | 10 | 46.6 | 26.2 | Hafifu |
| | | 16 | 5.8 | | |